

USHIRIKA

 Asante, Ndugu Orman. Tuna furaha usiku wa leo kuwa hapa ili kusikia ujumbe huu mzuri sana kutoka—kutoka kwa midomo ya ndugu yetu, ambaye tunaamini ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu kutuletea habari hizi kuu za, kama inavyosemwa, za maonyo: jinsi tunavyopaswa kuishi siku hii ya sasa katika utakatifu mbele za Mungu na mbele zetu sisi kwa sisi.

² Tu—tu—tunataka utakatifu tu miongoni mwetu ili kwamba mawasiliano machafu yasisikike miongoni mwetu hata kidogo tunapokiri wito huu mkuu wa Mungu. Hatuna budi kutembea inavyostahili kitu hiki ambacho Mungu ametuletea. Pia tuko huko chini kabisa tukielekea mwisho wa safari sasa, ambako tunatarajia mambo mengi sana na kwa wingi kuliko yale tungeweza kufanya ama kuwazia.

³ Pia kumbukeni, tunataka kuwa daima katika maombi. Na zaidi ya yote, yaangalie maisha yako: ikiwa maisha yako hayaendani na utakatifu wa Mungu, basi rudi na uanze kuomba tena; kuna kasoro. Unaona? Hatuna budi kuishi katika hali ambapo matunda ya Roho yatajitambulisha Yenyewe kupitia kwetu. Hivyo ndivyo tunavyotaka kuishi.

⁴ Mnajua, wakati mwingine tunawasikia wahubiri mashuhuri wanaoweza kuhubiri kwa nguvu sana, bali afadhali tuone mahubiri yakiishiwa kuliko kusikia yakihubiriwa, mnaona, naam, maana huo ndio ushahidi kwamba Mungu yuko ndani.

⁵ Sasa, tuna... tunakuja kwenye meza ya ushirika. Na sasa, hata hivyo, kuna wengine ambao hawali Ushirika, na labda wanaula tu kwenye makanisa yao wenyewe, bali tungefurahi usiku wa leo kama mngeweza, tungetaka, mshiriki nasi katika mambo haya. Hatuweki mipaka yoyote kwamba ni nani, mradi tu unaenenda kama inavyostahili—inavyostahili Injili ambayo una—unaisikiliza, na kukiri kuwa u sehemu yake.

⁶ Unajua wewe ni sehemu ya Injili hii. Wewe ni—wewe ni waraka ulioandikwa wa yale tunayozungumzia. Maadamu tunafanya jambo ambalo linaleta aibu, basi sisi ni aibu kwa yale tunayosikiliza. Mnaona? Hatuna budi kuishia yale tunayoamini, na kuyaishi hivi kwamba haitaleta aibu, bali tumuakisi Yesu Kristo katika mambo yote tunayofanya na kusema. Hivyo ndivyo ilivyo. Tunampenda tu kwa sababu hii.

⁷ Na sasa, usiku wa leo, tutasoma utaratibu wa meza ya Bwana unaopatikana katika Wakorintho wa Pili, yapata mlango wa 11. Nasi tusome hili na kumwacha tu kila mtu binafsi... jinsi tunavyofanya hili, endapo kuna wageni miongoni

mwetu, tunawaita watu kuyazunguka madhabahu m—mfululizo wanapoingia, kula Ushirika. Na kila Mkristo anastahili.

⁸ Sasa, kama unaishi maisha ambayo yanathibitisha jinsi ulivyo...Unataka kuuchunguza moyo wako. Kwa maana, hebu nihakikishe kutaja jambo hili, ambalo Maandiko yanasema hapa, “Kama tukiula isivyostahili.” Sasa, tunajua kwamba hatustahili sisi wenyewe; hakuna hata mmoja wetu anayestahili. Lakini kwamba hatutumaini ustahilifu wetu wenyewe, tunamtumainia Yeye aliye na...Tu—tunatumainia ustahilifu Wake, kwamba tumekufa kwa mawazo yetu wenyewe, na kuwazia tu mawazo Yake, na kuishia kila kitu ambacho tunaamini Yeye anatuamuru kufanya, na kuangalia nyuma na kuona kile tunachoishi, na kuyachunguza maisha yetu kabisa, na ikiwa tunafanya mambo ambayo hayaistahili Injili, basi hatupaswi kula Ushirika.

⁹ Lakini ikiwa tunafanya mambo ambayo tunafikiri kwamba...kwamba maisha yetu yanaweza kusomwa na watu wote, kwamba ikiwa mtu yeyote hangeweza kuelekeza kidole na kusema, “Nilimwona mtu huyu kwenye chumba cha baa hivi majuzi,” “Ni—nilimsikia mwanamume huyu akisimama na kutoa mizaha michafu,” “mwanamke huyu akifanya makosa,” basi, kama unajua ya kwamba huyo ni Roho Mtakatifu akikuelekeza kidole, basi usile Ushirika. Lakini kama wewe—kama unahisi kwamba—kwamba unaishi, kwamba ungeangalia nyuma na kuona kwamba dhambi zako zote zimeungamwa na ziko chini ya Damu, basi u—unapaswa kuula huo. Wewe—wewe ni—wewe ni sehemu yake.

¹⁰ Sasa, hebu na tusome Maandiko kama vile tu Mtakatifu Paulo anavyotuonya hapa katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu wa, samahani, katika Kitabu cha Wakorintho wa Kwanza m—mlango wa 11, kuanzia kifungu cha 23:

*Kwa maana mimi nimepokea kwa Bwana...
niliyowapa ninyi, Ya kuwa Bwana Yesu usiku ule
ule...aliosalitiwa alitwaa mkate:*

Laiti ningelikuwa na wakati wa—wa kuzungumzia hayo kidogo.

*...usiku ule ule aliosalitiwa (Mnaona?), yeye
alichukua mkate:*

*Naye alipokwisha kushukuru, akaumega, . . . akasema,
Twaeni na mle: huu ndio mwili wangu uliovunjwa kwa
ajili yenu: fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*

*Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe,
akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu
yangu: fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho
wangu.*

Kwa maana kila —mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.

Basi kila aulaye mkate huu, na kukinywea kikombe hiki cha Bwana, isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.

Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.

Maana alaye na kunywa isivyostahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili wa Bwana.

Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, . . . watu kadha wa kadha wamelala.

Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.

Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.

¹¹ Naomba nilete wazo hilo: tunapohukumiwa na Neno, ambalo ni Kristo, tunarudiwa. Ikiwa tunafanya makosa, hatuishi kulingana na Neno hili, tunarudiwa na Bwana. Na wakati Bwana *anapoturudi*, hiyo inamaanisha “kuturekebisha” sisi, isije ikatupasa adhabu pamoja na ulimwengu.

¹² Sisi si wa ulimwengu. Sisi ni tofauti na ulimwengu, tunaishi maisha tofauti, maisha yaliyotengwa. Hatupaswi kamwe kuishi maisha ya ulimwengu na kuwa Mkristo. Tunapaswa kuishi ma—maisha bora sana, maisha tofauti. Sio, simaanishi, katika wadhifa wa kijamii, lakini ninamaanisha tunapaswa kuishi maisha halisi ya utakatifu halisi ili matunda ya Roho yaonekane ndani yetu: ya upole; na unyenyekevu; na subira; uvumilivu; imani: tunda la Roho.

¹³ Lakini tunaposikia mambo haya, basi tunajua kwamba tumerudiwa na Bwana, kwamba tusiyaifanye, ndipo tunahukumiwa. Na ikiwa hatuna hukumu ndani yetu, kwamba tunaishi juu ya kitu hicho, kwa neema ya Mungu, basi hatuhukumiwi pamoja na ulimwengu, bali tunaishi juu ya mambo ya ulimwengu. Mnaona?

Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, ngojaneni.

Mtu akiwa na njaa, na ale nyumbani kwake; ili msipate kukutanika kwa hukumu. Na hayo yaliyosalia nijapo nitayatengeneza.

¹⁴ Daima tumeonyana sana juu ya hili, kwamba tunapokutanika, ingawa hatuwezi kuona kitu, kunaweza kuwa na kitu ndani ya mtu mwingine ambacho tunaona ambacho hakikuwa sahihi. Mnapokutanika kula Ushirika huu, ngojaneni, ombeaneni. Omba kwamba . . . Daima tunafanya

haya: nitakuombea kwamba ikiwa wewe, ikiwa kuna dhambi ndani yako ambayo, tendo ovu au kitu ambacho umefanya kama mwaminio, na—naomba ya kwamba Mungu atakuondolea, kwamba atakusamehe hicho. Nawe unaniombea kwamba endapo ja—jambo fulani ambalo nimefanya, ambalo sijui kulihusu, kama nimelifanya, na—na nilijua ni kosa, ningeninii, nitalikiri sasa hivi. Ninajiandaa kulikiri, kwa sababu aulaye na kukinywea isivyostahili, hula na kunywa hukumu kwa nafsi yake, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana.

¹⁵ Ule utambuzi wa kujua ya kuwa wewe ni mwili wa Bwana, huwezi kuutambua katika—katika uovu na dhambi; inabidi tuwe juu ya hayo. Kwamba tunatambua kwamba Bwana ni mwenye haki, na tunatambua kwamba Yeye ndiye Upatanisho wetu; kwamba dhambi zetu zote tumeziungama, na tunamwamini Yeye kwa kuungoja upatanisho Wake kutusafisha na uovu wetu wote; ndipo tunaupambanua mwili wa Bwana jinsi ulivyo, kupambanua kwamba ni wa nini.

¹⁶ Kisha tukitambua tena, kwamba ndani yetu, kama mwili wa Bibi-arusi wa Bwana, hebu tutambue kama kuna jambo lolote baya kwetu humu ndani ambalo lingezuia Injili kukua, au Bwana asitulete mbele za Mungu kama bikira safi. Hebu tutambue hilo sasa hivi na tuone kama ni makosa. Hebu tuyakiri ikiwa ni makosa. Hebu—hebu tuseme, “Bwana, ni—ninalisikitikia hilo.”

¹⁷ Kwa hiyo basi, huenda ikawa ni jambo ambalo tumefanya, umefanya, jambo ambalo nimefanya. Huenda si kwa kufahamu, sasa hivi, hebu tumwombe Mungu atusamehe hilo. Tulikuwa tunaimba wimbo hapa:

Samehe dha—dhambi nilizoiungama Kwako;
Samehe dhambi ya siri...?...mnaona;

Ambazo hata hawajui chochote kuihusu, dhambi isiyojulikana, tu—tu—tunaomba, “Mungu, wasamehe.”

¹⁸ Sasa, lilisema, “Mnapokutana, ngojaneni,” na kwa kweli hiyo ingekuwa hivi: ngojaneni. *Ngojaneni* inamaanisha “kusubiri,” subirianeni. Hebu tufanye hivyo sasa. Nitakuombea. Ikiwa unajua chochote ambacho umekosea, sema, “Mungu, nisamehe, sikumaanisha hilo, na kama utanisaidia tangu usiku huu na kuendelea, sitafanya hivyo tena. Na—namaanisha, Bwana, sitafanya hivyo tena kama utanisamehe tu. Na nikiisha kuungama ‘Naamini umenisamehe,’ ninaenda kuula mwili wa Kristo, nikihisi moyoni mwangu kwamba umenisamehe dhambi zangu zote.” Ninaombea basi dhambi yako ya siri, nawe ombea yangu, kwamba labda jambo fulani tusilojua, kwamba tusije pamoja ikatupasa adhabu pamoja na ulimwengu.

¹⁹ Hatutaki ulimwengu humu. Sehemu hii ndogo ya watu ambao Mungu ametupa tuabudu pamoja nao hapa, tunataka kujiweka safi kutokana na ubinafsi, kuweka kitu chetu...

dhambi zetu... maisha yetu safi kutokana na mambo yote ya ulimwengu, ili tusitiwe doa na hayo. Tunataka kuwa tayari kwa ajili ya Unyakuo.

Kwa hiyo na tuombeane sasa, kimya, sisi kwa sisi, kwa muda kidogo tu. Mniombea ninapowaombea.

²⁰ Bwana Yesu, na iwe, Bwana, kwamba dhambi zetu zote ziwe sasa katika Damu ya Bwana Yesu, katika usahaulifu wa kumbukumbu za Mungu, kwamba tuje pamoja sasa kama waaminio wapendwa na watoto katika Kristo, kwa maana tunaomba hilo, katika Jina Lake. Amina.

²¹ Sasa, wakati huu wakati wa—wazee, nafikiri waje mbele. (Je, huo ungali ndio utaratibu, hapa?) Ndugu Tony Zabel, naye atawaelekeza. Na kama kuna yeyote anayepaswa kuondoka sasa wala hataki kubaki kwa ajili ya Ushirika, tuna furaha kuwa nawe usiku wa leo. Kumbuka mkutano wetu wa Jumatano... Mkutano wa maombi ya Jumatano usiku. Nawe ondoka kimya wakati hao wengine wanapokuja madhabahuni. Naye Ndugu Zabel, hapa, atawaongoza wa—watu madhabahuni tunapoutayarisha Ushirika.

²² Huu unawakilisha mwili wa Bwana Yesu, Mkate. Na kama vile ule wimbo ulivyoimbwa hivi punde, *Imani Yangu Inakutazama*. Kuna maagizo matatu tu ambayo Bwana alikuwa ametupa, na hayo yalikuwa ni ubatizo, kula mkate na divai, na kutawadha miguu, ndiyo hayo maagizo. Nao huu unawakilisha mwili wa Kristo uliovunjwa.

²³ Maombi yangu ni kwamba kila mtu anayeushiriki huu usiku wa leo, kwamba, watapokea baraka za Roho Mtakatifu kuja juu yao. Na kwamba wao ni wagonjwa, Mungu wa Mbinguni, Yeye aliyeanzisha huu katika mfano wa kwanza huko Misri kwa kula mbo—mboga zenye uchungu pamoja na divai, ninatumaini ya kwamba Mungu atawaponya, na katika safari yenu yote hakutakuwako na magonjwa miongoni mwenu. Mungu wa Mbinguni na atutazame sasa, tunapomtolea huu.

²⁴ Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, na Mpaji wa kila kipawa chema, tunakushukuru kwa ajili ya utaratibu huu, kwamba tungeweza kufanya hivi kwa ukumbusho Wako tunapofanya ushirika, tuseme, Mbele Zako, kwenye ushirika wa neema ya Mungu. Tunapowazia ndani ya mioyo yetu wenyewe, kwamba siku moja tulikuwa hatukustahili, na sasa Damu ya Yesu Kristo imetusafisha na dhambi hiyo, hata tunasimama pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu.

²⁵ Mkate huu wa kosha, Baba, ambao umeokwa na kuletwa hapa kwa kusudi hili, ambao tunakuomba uutakase, Bwana, kwamba katika uwakilishi wa mwili uliovunjika... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] kama utakatifu na uchungu na mateso ambayo Yeye aliteseka pale Kalvari wakati mwili

huu ulipovunjwa. Kwamba alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Ndiyo maana tunakula mkate huu uliovunjika usiku wa leo. Mungu awabariki waaminio na autakase mkate huu—huu mwembamba uwe mfano wa mwili wa Yesu Kristo. Amina.

²⁶ Biblia ilisema, “Vivi hivi akakitwaa kikombe, na alipokwisha kula, akatwaa, kasema, twaeni mnywe, hiki ndicho kikombe cha Agano Jipya; kila mnapofanya hivi, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.” Ninapoishika mkononi mwangu usiku wa leo divai hii, iliyotengenezwa kutoka kwa—kutoka kwa uhai wa zabibu ambazo zimeletwa pamoja hapa kuwakilisha Damu ya Yesu Kristo, hakuna wakati bado, ambapo nimewahi kuchukua sinia ya ushirika, pasipo kutazama mle ndani na kuona dhambi zangu zimeondolewa. Naona kama isingalikuwa kwa sababu hiyo, kile—kile... vema, tungekuwa wapi?

²⁷ Ninawazia mle ndani ambapo mgonjwa alikuwa akifa, kule hospitalini: mimi. Ni kwa kupigwa Kwake mimi niliponywa. Mungu wa Mbinguni na aibariki divai hii kwa matumizi iliyokusudiwa.

²⁸ Bwana Yesu, tunakuletea maji haya ya zabibu, divai iliyotolewa kutoka kwa damu ya zabibu kuwakilisha Damu ya Yesu Kristo. Jalia, tunapoipokea, Baba, jalia magonjwa yatuondokee. Jalia dhambi, tamaa, ziondolewe kwetu. Jalia tuishi maisha matakatifu, yaliyowekwa wakfu baada ya haya, hata watu waone uakisi wa Yesu Kristo ndani yetu, na kwamba matembezi ye—yetu maishani yaistahili Injili tunayoamini. Tujalie, Baba. Pia takasa... divai hii sasa, kwa matumizi yake yaliyokusudiwa. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina. 

63-0707^E Ushirika
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org